# CHUO KIKUU CHA TUMAINI MAKUMIRA

**OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO**

**S.L.P 55, USA-RIVER, ARUSHA**

## SHEREHE YA MAHAFALI

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira anapenda kuwataarifu wahitimu wote wa mwaka wa masomo 2022/2023 na wananchi wote kwa ujumla kuwa Mahafali ya 67 LTCM, ya 27 MUCo na ya 13 TUMA yatafanyika siku ya Jumamosi tarehe 25 Novemba, 2023 katika viunga vya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Arusha kuanzia saa tatu kamili (3:00) Asubuhi. Wahitimu wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Majoho yatatolewa kuanzia tarehe 22 Novemba, 2023 kuanzia saa nane kamili (8:00) mchana mpaka saa kumi na nusu (10:30) jioni.

2. Wahitimu wanalazimika kuhudhuria Jumuiko la Kitaaluma (Convocation) na mazoezi ya maandalizi ya mahafali (Rehearsal) siku ya Ijumaa tarehe 24 Novemba, 2023 kuanzia saa tatu kamili (3:00) Asubuhi. Kadi maalumu zitatolewa kwa wahitimu wakati wa mazoezi ya maandalizi ya mahafali. Wahitimu watakaokuwa na kadi maalumu tu ndio watakaoruhusiwa kuingia katika eneo la mahafali siku ya tarehe 25 Novemba, 2023.

3. Faini ya shilingi za Kitanzania 20,000/= itatozwa kila siku kwa wahitimu watakaorudisha majoho baada ya tarehe 30 Novemba, 2023.

4. Wahitimu wote watakaohudhuria katika mahafali wanakumbushwa kuzingatia utaratibu wa mavazi wa chuo, na kujigharamia kwa usafiri, chakula na malazi.

Aidha, Makamu Mkuu wa Chuo anapenda kuwaalika “ALUMNI” wote katika Jumuiko la Kitaaluma (Convocation) litakalofanyika siku ya Ijumaa tarehe 24 Novemba, 2023 kuanzia saa tatu kamili (3:00) Asubuhi.

WOTE MNAKARIBISHWA

*Imetolewa na:*

Makamu Mkuu wa Chuo
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira